

ASb  
approved




Kiswahili


# Akili ni mali

## Ursula Nafula


### Abraham Muzee




Sokwe alimkuta  
Mamba kando ya  
mto mkubwa.




Mamba akasema,  
"Nina maumivu.  
Tafadhali nisaidie."



Sokwe akamuuliza,  
"Unahitaji nini?"




Mamba akamjibu,  
"Usiponipatia  
moyo wako,  
sitapona."




Sokwe akasema,  
"Kwanza nibebe  
hadi upande wa  
pili wa mto."



Mamba akambeba  
Sokwe mgongoni  
wakavuka mto.




Sokwe akasema,  
"Ninahitaji kisu ili  
nikate moyo  
wangu."




Wakati huo huo,  
upepo mkali  
ukaanza kuvuma.




Mamba akainuliwa  
juu karibu  
amuangushe  
Sokwe.



Sokwe alipoiona  
nchi kavu,  
akamwambia  
Mamba  
aharakishe.



Ghafla, Sokwe  
akaurukia mti.



Mamba  
akakasirika  
akasema,  
"Ulinidanganya!  
Utajuta!"

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

## Akili ni mali

Author - Ursula Nafula

Illustration - Abraham Muzee

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2017

Creative Commons: Attribution 4.0

Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)

